



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TANGAZO LA MWALIKO WA WAANGALIZI WA NDANI WA UCHAGUZI MKUU
WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI WA MWAKA 2025**

Kwa mujibu wa kifungu cha 85(4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kikisomwa pamoja na kanuni ya 13(1) na (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2024, Tume inawaalika waangalizi wa ndani wa uchaguzi wenye nia ya kutazama Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025.

Kupitia tangazo hili, Tume inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi mbalimbali nchini ambazo zinahitaji kutazama Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Maombi hayo yawasilishwe kupitia Mfumo wa Usajili wa Waangalizi (AMS) kwa kutumia kiunganishi (*link*) <https://ams.inec.go.tz>

Maombi yanatakiwa kuainisha mambo yafuatayo: -


- i. anuani ya taasisi au asasi husika;
- ii. mahali ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi;
- iii. shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;
- iv. sehemu ambazo taasisi au asasi inapenda kwenda kuangalia uchaguzi;
- v. idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na majina na taarifa zao binafsi;
- vi. majina na namba za simu za viongozi wa taasisi au asasi husika;
- vii. ikiwa taasisi au asasi ya ndani inahusisha viongozi ambao si raia wa Tanzania, viongozi wawili ni lazima wawe watanzania;
- viii. kuambatisha nakala au kivuli cha hati au nyaraka ya usajili wa taasisi au asasi husika; na
- ix. kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.

Maombi yatakayozingatiwa na Tume ni yale tu yatakayowasilishwa kupitia kiunganishi (*link*) kilichowekwa katika tangazo hili yaani <https://ams.inec.go.tz>

Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe 21 Aprili hadi 20 Mei, 2025.

Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la uangalizi kwa taasisi au asasi zitakazopewa kibali.

Imetolewa leo tarehe 21 Aprili, 2025 na:



Kailima, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI